





# NJIA YA MSALABA

# TAFAKARI YA MT. PADRE PIO

## KITUO CHA KWANZA

**Yesu anahukumiwa afe.**

- Ee Yesu tunakuabudu, tunakushukuru.
- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa  msalaba wako mtakatifu.

Fikiri jinsi ambavyo Yesu alipigwa mijeledi na kuvikwa taji la miiba na kuhukumiwa na Pilato bila ya  kosa lolote, afe juu ya msalaba.

"Bwana wetu mwenye huruma anakuja kwa upendo kunisaidia wakati wa majaribio makubwa sana na kama baba mwenye upendo, ananifariji na kuniimarisha mara kwa mara katika njia ya msalaba."

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

*K. Ee Bwana, utuhurumie W. Utuhurumie*

*K. Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani. W. Amina.*

## KITUO CHA PILI

**Yesu anapokea msalaba.**

- Ee Yesu tuakuabudu,tunakushukuru,
- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa msalaba wako mtakatifu.

Fikiri jinsi Yesu alivyokubali mbele ya Mungu kuchukua na kuelemewa na msalaba na kufia juu yake kwa ajili ya wokovu wetu.

"Situmaini kupunguziwa uzito wa msalaba wangu, kwa sababu ninaona furaha kuteseka pamoja na Yesu. Ninapotafakari msalaba juu ya mabega ya Yesu, naimarika na kushukuru kwa furaha takatifu."

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

***K.*** *Ee Bwana, utuhurumie* ***W.*** *Utuhurumie*

***K.*** *Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani.* ***W.*** *Amina.*

## KITUO CHA TATU

**Yesu anaanguka mara ya kwanza.**

- Ee Yesu tunakuabudu, tunakushukuru.
- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa msalaba wako mtakatifu.

Tafakari kuanguka kwa Yesu chini ya msalaba mara ya kwanza, akipigwa na askari, akiwa na taji la miiba kichwani na damu ikitiririka. Alisimama, akaubeba msalaba wake na kuendelea na safari ya ukombozi. Yesu alikuwa amedhoofika sana kwa kuwa askari walikuwa wanaendelea kumpiga bila huruma na aliaaguka mara kwa mara.

"Upendo wa dhati unajidhihirisha unapoteseka kwa ajili ya yule tunayempenda kama Mwana wa Mungu alivyoteseka kwa upendo wa dhati. Hakuna shaka kwamba msalaba uliobebwa kwa ajili yake unaweza ukalinganishwa sawa na upendo kwetu."

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

***K.*** *Ee Bwana, utuhurumie* ***W.*** *Utuhurumie*

***K.*** *Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani.* ***W.*** *Amina.*

## KITUO CHA NNE

**Yesu anakutana na Mama yake**

- Ee Yesu tunakuabudu, tunakushukuru.
- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa msalaba wako mtakatifu

Tafakari hali ya Mama Maria na Yesu walivyokutana na uchungu waliokuwa nao mioyoni mwao. Waliangaliana kwa mioyo yenye upendo iliyokuwa katika mateso makali na huruma nyingi.

"Ninamwomba Bikira wa Mateso atujulie kutoka kwa mwanae mtakatifu sana atuangazie kila mara neema ya maajabu ya msalaba na tuneemeshwe kwa mateso yake. Tunamwomba Bikira Mtakatifu atujalie upendo wa msalaba wa mateso na wa uchungu kwa kuwa yeye ni wa kwanza kuishi injili katika ukamilifu wake na katika mahangaiko yake, atujalie msukumo wa kumfuata mara."

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

***K.*** *Ee Bwana, utuhurumie* ***W.*** *Utuhurumie*

***K.*** *Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani.* ***W.*** *Amina.*

KITUO CHA TANO

**Simoni wa Kirene anamsaidia Yesu.**

- Ee Yesu tunakuabudu, tunakushukuru.
- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa msalaba wako mtakatifu

Tafakari hali aliyokuwa nayo Yesu aliposaidiwa msalaba na Simoni wa Kirene. Wayahudi walipoona Yesu anazidi kudhoofika walihisi angeweza kufa kabla ya kuwambwa mslabani. Hivyo walimlazimisha Simoni wa Kirene kuubeba msalaba wa Yesu.

"Yesu anajichagulia nafsi na kati ya hizi, ingawa mimi sistahjili amenichagua mimi kusaidia katika kazi ya kuwakomboa watu. Na kadri hizi nafsi zinavyoteseka bila kufarijika ndivyo zinavyozidi kufanya mateso ya Yesu yapungue. Ndiyo maana natamani sana kuteswa bila kufarijiwa na kwa jinsi hii Napata furaha."

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

***K.*** *Ee Bwana, utuhurumie* ***W.*** *Utuhurumie*

***K.*** *Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani.* ***W.*** *Amina.*

KITUO CHA SITA

**Veronika anapangusa uso wa Yesu.**

- Ee Yesu tunakuabudu, tunakushukuru.

- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa  msalaba wako mtakatifu

Tafakari ujasiri aliokuwa nao Veronika wa kupangusa uso wa Yesu bila ya kuogopa askari na jinsi alivyozawadiwa picha ya uso wa Yesu juu ya kile kitambaa.

"Kama nikijua mmojawapo ameumizwa kimwili au kiroho , nifanye nini mbele ya Bwana kumwona yule mtu ameondokana na maovu haya nitalazimika kwa  utashi wangu kuchukua mateso hayo. Nitajipatia matunda ya mateso haya, kama Bwana angeruhusu."

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

***K.*** *Ee Bwana, utuhurumie* ***W.*** *Utuhurumie*

***K.*** *Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani.* ***W.*** *Amina.*

KITUO CHA SABA

**Yesu anaanguka mara ya pili.**

- Ee Yesu tunakuabudu, tunakushukuru.
- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa  msalaba wako mtakatifu

Tafakari tendo la Yesu kuanguka mara ya pili chini ya msalaba na kujitonesha madonda aliyokuwanayo na kuamsha upya mateso aliyoyapata tangu mwanzo.

"Ndiyo, naupenda msalaba na ni msalaba tu. Naupenda kwa sababu kila mara nauona kwenye mabega ya Yesu. Sasa Yesu anaona moja kwa moja kuwa maisha  yangu na moyo wangu vyote vimeweka nadhiri kwake na mateso yake."

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

***K.*** *Ee Bwana, utuhurumie* ***W.*** *Utuhurumie*

***K.*** *Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani.* ***W.*** *Amina.*

KITO CHA NANE

**Akina mama wanamlilia Yesu.**

- Ee Yesu tunakuabudu, tunakushukuru.
- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa  msalaba wako mtakatifu

Tafakari kitendo cha wanawake  waliokuwa wanamlilia  yesu kwa huzuni walipokutana naye akiwa amebeba msalaba,na yale maneno aliyowaambia : Enyi binti wa Yerusalem, msinililie mimi, bali jilílieni nafsi zenu na watoto wenu."(***Luka 23:28)***

“Usiwe na hofu kwa kuwa muda wa majaribu ni mrefu sana. Ukombozi tunaufikia baada ya kuvuka bahari yenye dhoruba ambayo kwa kawaida huhatarisha imani yetu. Mlima wa Kalvari ni watakatifu lakini kutoka hapo tutaenda mlima mwingine unaoitwa Tabor.”

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

***K.*** *Ee Bwana, utuhurumie* ***W.*** *Utuhurumie*

***K.*** *Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani.* ***W.*** *Amina.*

## KITUO CHA TISA

**Yesu anaanguka mara ya tatu.**

- Ee Yesu tunakuabudu, tunakushukuru.
- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa msalaba wako mtakatifu

Tafakari kuanguka kwa Yesu chini ya msalaba mara ya tatu. Yesu alikuwa amedhoofika hawezi kutembea nguvu zilikuwa zinamwishia na askari waliendelea kumpiga bila huruma.

“Usisahau kwamba inapofika saa ya mateso ninakuwa mbinafsi, kwa kuwa nataka kuteseka peke yangu, licha ya kwamba sina subira kwenda kwa Kristu, inabidi nijilaumu kama niliomba nisiteseke angalau mara moja kwa muda, au mbaya Zaidi, kama wengine walijaribu kuchukua fadhila hii kutoka kwangu.”

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

***K.*** *Ee Bwana, utuhurumie* ***W.*** *Utuhurumie*

***K.*** *Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani.* ***W.*** *Amina.*

## KITUO CHA KUMI

**Yesu anavuliwa nguo.**

- Ee Yesu tunakuabudu, tunakushukuru.
- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa msalaba wako mtakatifu

Tafakari udhalimu aliofanyiwa Yesu wa kuvuliwa ngo zilizokuwa zimegandamana na madonda yake. Walizibandua kwa nguvu na kumtonesha madonda yake. Hawakuwa na huruma kwa Mkombozi wetu waliendelea kumfanyia vitendo vya ukatili.

"Yesu ananiambia kwamba katika upendo yeye ananifurahisha lakini katika huzuni mimi ninamfurahisha yeye. Anapohitaji nijue kwamba ananipenda, ananishirikisha katika madonda, miiba na mateso makali. Anaponitaka nifurahi anaujaza moyo wangu na roho moto."

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

***K.*** *Ee Bwana, utuhurumie* ***W.*** *Utuhurumie*

***K.*** *Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani.* ***W.*** *Amina.*

## KITUO CHA KUI NA MOJA

**Yesu anasulibishwa msalabani.**

- Ee Yesu tunakuabudu, tunakushukuru.
- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa  msalaba wako mtakatifu

Tafakari Yesu alivyowambwa kwenye mti wa msalaba kwa kupigiliwa misumari na kuachwa afe juu yake.

"Yesu pekee anaweza kuelewa ninavyoteseka, ninapojiandaa kwa ajili ya tukio la huzuni la Kalvari. Hakuna mtu anayeweza kuelewa nafuu anayoipata Yesu wakati mtu anaposhiriki siyo tu mateso yake, lakini pale ambapo nafsi ya upendo inaposhindwa kuomba huruma na kushiriki mateso."

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

***K.*** *Ee Bwana, utuhurumie* ***W.*** *Utuhurumie*

***K.*** *Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani.* ***W.*** *Amina.*

## KITUO CHA KUMI NA MBILI

**Yesua anakufa Msalabani**

- Ee Yesu tunakuabudu, tunakushukuru.
- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa  msalaba wako mtakatifu

Tafakari mateso na maumivu aliyoyapata Yesu juu ya msalaba kwa masaa matatu (3) mpaka alivyokata roho.

"Ni kwa jinsi gani lilivyo tamu jina la Msalaba! Chini ya Msalaba, nafsi zimevalishwa mwaga na kumulikwa na upendo. Hapa nafsi zinapokea mbawa ambazo zitazinyanyua

juu Zaidi. Tunaomba msalaba huu uwe kila mara kitanda chetu cha mapumziko, shule yetu ya ukamilifu, urithi wetu wa upendo. Mungu umenifanya niamini kuwa sitashuka juu ya msalaba kamwe."

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

***K.*** *Ee Bwana, utuhurumie* ***W.*** *Utuhurumie*

***K.*** *Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani.* ***W.*** *Amina.*

**KITUO CHA KUMI NA TATU.**

**Yesu anashushwa malabani.**

- Ee Yesu tunakuabudu, tunakushukuru.
- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa  msalaba wako mtakatifu

Tafakari kitendo cha Joseph na Nikodemu cha kuchukua mwili wa Yesu juu ya msalaba na kumpatia mama yake ambaye aliukumbatia kifuani mwake.

"Ninajua vyema kwamba msalaba ni ahadi ya upendo, msalaba ni dhana ya msamaha na upendo ambao haujalishwa na kushibishwa na msalaba siyo upendo wa kweli. Nina hamu kubwa kuteswa kwa ajili ya upendo wa Yesu."

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

***K.*** *Ee Bwana, utuhurumie* ***W.*** *Utuhurumie*

***K.*** *Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani.* ***W.*** *Amina.*

**KITUO CHA KUMI NA NNE.**

**Yesu anazikwa kaburini.**

- Ee Yesu tunakuabudu, tunakushukuru.
- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa  msalaba wako mtakatifu

Tafakari kitendo cha mitume kubeba mwili wa Yesu kwenda kuzika; wakiwa na mama yake ambaye aliuweka mwili wa mwanae kaburini kwa mikono yake.

"Natamani kufa au kumpenda Mungu, ama kifo au Upendo, kwani maisha bila upendo ni mbaya Zaidi ya kifo."

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

***K.*** *Ee Bwana, utuhurumie* ***W.*** *Utuhurumie*

***K.*** *Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani.* ***W.*** *Amina.*

KITUO CHA KUMI N TANO

**Yesu amefufuka.**

- Ee Yesu tunakuabudu, tunakushukuru.
- Kwa kuwa umewakomboa watu kwa msalaba wako mtakatifu

Tafakari kuwa mwenye dhambi au kutokuwa na dhambi pekee siyo muhimu kabla ya muujiza wa Kristu. Jambo muhimu ni kuwa na Imani na matumaini tunapokuwa tunashuka mlima Kalvari tukiwa na mioyo iliyofunguka kwa upendo wa Kristu; tunaweza kushuka mlima Golgota pamoja na Maria kama hatuna dhambi na kuzitibu na kubadilika kuelekea kwenye ufufuko na kukutana na Baba yetu wa mbinguni.

"Usiogope shida, kwa sababu hiyo nafsi yako inawekwa chini ya msalaba ambao utakupeleka hadi kwenye milango ya mbingu, ambao utamkuta yule aliyeshinda kifo, ambaye atakutambulisha kwenye furaha ya milele….. **Mateso makali ya Kristu inabidi yawe akilini mwako kama unataka kushiriki katika ushindi wake.**"

*Baba yetu – Salamu Maria – Atukuzwe Baba.*

***K.*** *Ee Bwana, utuhurumie* ***W.*** *Utuhurumie*

***K.*** *Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa Amani.* ***W.*** *Amina.*

*REJEA:*

*Sala na Novena kwa Mt. Pd. Pio: Na:St. Paulines*

***Aveee!***

***"Mapendo ni ya Milele."***

***F. Masaka***